

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA



Mawasiliano:
Simu: 0272-970677
Nukushi: 027-2970678
Baruapepe:
ded@sihadc.go.tz
Tovuti: www.sihadc.go.tz

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
5 BR-Sanya Juu-Elerai
S.L.P 129,
25482 SIHA.

Unapojibu tafadhali taja:
Kumb.Na. SDC/B.20/7/124

Tarehe: 20/04/2023

TANGAZO LA NAFASI YA KAZI YA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Siha amepata kibalizi cha Ajira ya Mkataba cha kuajiri Fundi sanifu (Magari) kutoka kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi na Umma na Utawala Bora cha Kumb. Na.FA.97/228/02"A"/27 cha tarehe 15 Februari, 2023.

Nafasi hiyo ni Ajira ya Mkataba wa mwaka mmoja (Renewable) kama ifuatavyo:-

1. Fundi Sanifu II (mechanical): Nafasi 01

SIFA ZA MWOMBAJI:

- i. Waliohitimu kidato cha Sita na kufuzu Mafunzo ya Ufundi ya miaka miwili kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali katika moja ya Fani za Ufundi.
- ii. Waliohitimu kidato cha Nne na kufuzu kozi ya Ufundi ya miaka mitatu kutoka Vyuo vya Ufundi vinavyotambulika na Serikali katika moja wapo ya Fani za ufundi.
- iii. Wenye Cheti cha majaribio ya Ufundi hatua ya kwanza kutoka Chuo cha Ufundi kinachotambuliwa na Serikali.
- iv. Wenye Stashahada ya kawaida katika Fani ya ufundi kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

MAJUKUMU YA KAZI

1. Kukagua Magari yote ya Halmashauri na kushauri endapo yanahitaji matengenezo.
2. Kuhakikisha Magari yote yanafanyiwa matengenezo muda wa matengenezo unapofika.
3. Kutoa ushauri wa kiufundi kuhusu utunzaji wa Magari.

4. Kufanya na kusimamia kazi za Ufundi katika karakana ya Halmashauri.
5. Kutunza Vifaa, Vipuli na Zana za Magari yote ya Halmashauri.
6. Kusimamia Sheria, Sera na Kanuni zinazohusu matengenezo ya Magari ya Serikali.

NGAZI YA MSHAHARA:

Mwombaji atakayefanikiwa kujiunga kwa Cheo cha Fundi Sanifu II (Magari) atalipwa Mshahara ngazi ya TGS B₁ Kwa mwezi.

SIFA ZA JUMLA ZA MWOMBAJI

1. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 hadi miaka 45.
2. Waombaji wote waambatanishe nakala za vyeti vya Elimu, Taaluma, Cheti cha kuzaliwa na picha Ndogo mbili za rangi za hivi karibuni (Passport size) pamoja na nakala ya Kitambulisho cha Nida au namba ya Nida.
3. Waombaji wote waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza (CV).
4. Waombaji watakaokidhi sifa wataitwa kwenye Usaili
5. Waombaji watakaoitwa kwenye Usaili watatakiwa waje na vyeti halisi (Original Certificates)
6. Nakala za vyeti zisainiwe na kupigwa muhuri na Mwanasheria/ Wakili wa Serikali au Mahakama.

UTARATIBU WA KUTUMA MAOMBI

Maombi yote yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

MKURUGENZI MTENDAJI,
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA,
5 BR-Sanya Juu-Elerai
S.L.P 129,
25482 SIHA - KILIMANJARO

N:B Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **02/05/2023** saa tisa na nusu Alasiri.

Mangali U.E

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIHA**

MKURUGENZI MTENDAJI (W)

SIHA

Nakala: Katibu,
Sekretarieti ya Ajira
katika Utumishi wa Umma,
Jengo la Utumishi (UDOM),
Eneo la Dkt. Asha Rose Migiro,
S.L.P 232
DODOMA.